



Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra

Embassy of Switzerland in Tanzania
Ubalozi wa Uswisi Tanzania

9 February 2016

UBALOZI WA USWISI WAANDAA MDAHALO WA WAZI KUHUSU AJIRA KWA VIJANA

Taarifa Kwa Vyombo Vya Habari

Mwaka huu ni maadhisho ya miaka 50 ya mahusiano na ushirikiano baina ya Uswisi na Tanzania. Kama sehemu ya mipango ya kusheherekeea maadhisho haya, Ubalozi wa Uswisi leo umeandaa mdahalo wa wazi kuhusu ajira kwa vijana katika hoteli ya Coral Beach jijini Dar es Salaam.

Karibu theluthi mbili ya Watanzania wana umri chini ya miaka 25. Hii inatoa fursa kubwa kwa rasilimali watu. Ili kutumia kikamilifu nafasi hii, ni muhimu kuwekeza katika ujuzi na elimu kwa vijana. Utafiti wa hivi karibuni wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) unaonyesha kuwa 21.1% ya vijana (miaka 15-29) hawana ajira, ambayo ni kiwango cha juu ukilinganisha na nchi nyingine Kusini mwa Sahara.

Zaidi ya vijana 800,000 wanaingia katika soko la ajira kila mwaka hapa Tanzania, lakini ni wapatao 40,000 tu kati yao ambao hupata ajira rasmi. Mtazamo wa soko la ajira bado ni hasi, hasa kwasababu ya ukosefu wa wafanyakazi wenye ujuzi na kutokuwa na uwiano kati ya ujuzi ugavi na mahitaji. Kwasababu hizi, suala la ajira linapewa kipaumbele na wadau wote.

Mdahalo huu unaangalia changamoto hii na kupendekeza njia mbalimbali za kukabiliana nayo kupitia majadiliano yanayojumuisha karibia wawakilishi 80 kutoka sekta za umma na binafsi, vijana, asasi za kiraia na washirika wa kimataifa. Kati ya mambo muhimu yatakayojadiliwa ni pamoja na mifumo ilivyofanikiwa sehemu zingine. Hii ni pamoja na mifumo wa elimu wa Uswisi (VPET - Swiss Vocational and Professional Education and Training) ambao kwa kushirikiana na sekta binafsi, huwezesha vijana kuijunga kwenye mafunzo ya miaka miwili mpaka minne inayochanganya mafunzo ya kazi kwa nadharia na vitendo, na usoefu wa kazi kwenye makampuni binafsi.

Mdahalo umeendeshwa na Aidan Eyakuze, Mkurugenzi Mtendaji wa Twaweza. Washiriki wengine ni pamoja na Bw. Hassan Mshinda, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH); Bi Mary Kawar, Mkurugenzi wa ILO na Bw. Thomas Katebalirwe, Mkurugenzi TVET, Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi. Wengine ni pamoja na wawakilishi kutoka taasisi za umma na binafsi, asasi zisizo za kiserikali na wadau wa kimataifa.

Ubalozi wa Uswisi kupitia shirika lake la maendeleo (Swiss Development Cooperation - SDC) tayari inachangia pamoja na shirika la MasterCard Foundation kwenye mradi wa fursa za ajira kwa vijana "Opportunities for Youth Employment - OYE" ambao unalenga kuongeza ajira na mapato kwa vijana kupitia ufundi stadi na stadi za maisha.

Kabla ya mdahalo huu wa wazi, uwakilishi wa Mabalozzi wa Uswisi pamoja na Wakuu wa shirika la lake la maendeleo kutoka nchi za Kusini na Mashariki ya Afrika wametembelea maeneo mbalimbali ili kuelewa zaidi hali ya ajira ya vijana Tanzania. Sehemu walizotembelea ni pamoja na Buni Innovation Hub (COSTECH), mwajiri mmoja wa sekta binafsi anayeajiri wahitimu wa VETA (Vocational Education and Training Authority), na wameshiriki kwenye mkutano na vijana chuo kikuu cha Dar es Salaam.